Hekima, Umoja, Amani, Ni ngao Zetu!

Jumatatu 28 Novemba, 2022

# NCHI YETU

*Tanzania imara, Kazi Iendelee*

www.maelezo.go.tz | Toleo la 420 | Idara ya Habari MAELEZO | TANZANIA

## 28 NOVEMBA 2022




HALIUZWI

# TAHARIRI

# Tuungane Kukemea Uharibifu wa Mazingira

Mmoja wa wasanii wakongwe hapa nchini aliwahi kuimba wimbo unaeleza kuhusu jambo ambalo kwa sasa limeleta athari kubwa hasa kupeleka mabadililo ya tabia ya nchi na hivyo kuathiri shughuli mbalimbali za maendeleo katika Taifa letu.

Msanii huyo katika sehemu ya wimbo wake anasema "Mazingira yetu tunayaribu na dunia yetu inaangamia" ni wazi kuwa uhabirifu wa mazingira kwa sababu ya shughuli za kibinadamu umepelekea adha kubwa kwa watanzania walio wengi hasa kipindi kirefu cha ukame kwa maeneo mengi.

Wanaoharibu mazingira kwa kuchoma moto misitu, kukata miti ovyo, kuchepusha mito kwa shughuli za kilimo, ufugaji na nyingine nyingi hakika wanaguswa na msanii huyu na anawataka kuacha mara moja tabia hii kwani athari zake ni za muda mrefu na zitapelekea kushuka kwa shughuli za uzalishaji na ukuaji wa uchumi.

Jambo hili si la kuvumiliwa kamwe kwani hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan naye amekea vikali tabia hii ya uaharibifu wa mazingira kwa nyakati tofauti mfano hivi karibuni wakati akizindua mradi wa maji Kigamboni jijini Dar es Salaam alieleza kinaga ubaga kuwa upungufu wa maji katika Jiji la Dar es Salaam unasababishwa na shughuli za kibinadamu katika mikoa ya Pwani na Morogoro ikiwemo wafugaji wenye makundi makubwa ya mifugo, wachimba madini, wale wanaokata miti katika safu za Milima ya Uluguru  na wengine wanaochepusha maji  ya mito inayopeleka maji katika Mto Ruvu ambao ni chanzo cha maji kwa jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani.

Chakujiuliza hapa ni je ubinafsi huu wa watu wachache wanaoharibu mazingira una faida kwa Taifa? Jibu lake ni kuwa ubinafsi huu hauna faida zaidi ya kuleta madhara kwa kizazi cha sasa na kijacho hivyo lazima upigwe vita na Viongozi wa Dini, Serikali na kila mpenda maendeleo katika Taifa letu.

Kila anayeharibu mazingira ni wazi kuwa amekosa uzalendo kwa Mama Tanzania ambaye  kwa hakika lazima alindwe na kutunzwa kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aidha, kwa sasa ubinafsi  huu unaathiri malioni ya Watanzania kutokana na kukosekana kwa maji yakutosheleza mfano jiji la Dar es Salaam kwa sasa linapata maji kwa mgao kwa sababu ya athari za uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu wachache.

Serikali ya Awamu ya Sita inachukua hatua za makusudi katika kuhakikisha kuwa jiji hilo ambalo ni la kibishara linakuwa na maji ya uhakika ndiyo sababu Rais akaagiza kuwa mradi wa uchimbaji visima Kimbiji na Mpera ukamilke na pia ujenzi wa Bwawa la Kidunda uanze.

Pia, katika maeneo yote Serikali imewekeza fedha nyingi katika kutekeleza miradi ya maji ambayo kwa kiasi kikubwa inategemea utunzaji wa mazingira ili iweze kuwa endelevu, hivyo suala hili halina mbadala wake.

Utekelezaji wa miradi hiyo utakuwa na tija kama utunzaji wa mazingira utazingatiwa katika Taifa letu, Taasisi za mazingira na wadau wote tuungane na Rais wetu katika hili na tutafanikiwa kutokomeza vitendo hivi.

Mpita njia anawaomba Watanzania wote pale walipo kuamka na kuungana katika Kampeni hii iliyoanzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha kuwa unaribifu wa mazingira unakomeshwa katika maeneo yetu, kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake ili tuweze kufikia azma ya Rais wetu mpendwa kujenga Taifa lenye ustawi unaoenda sambamba na utunzaji wa mazingira kwa kutoa kipaumbele kwa mazingira yetu katika kila jambo.

Ni wazi kuwa tukiungana kwa pamoja tutawashinda hawa wachache wanaoharibu mazingira yetu ambayo ni urithi, tunapaswa tuwarithishe na vizazi vijavyo. Ukataji wa miti ovyo lazima nao ukomeshwe katika maeneo yetu, hapa viongozi katika ngazi mbalimbali mnalo jukumu la kusimamia suala hili kwa manufaa ya Taifa, hivi karibuni Mpita njia amejionea uharibifu mkubwa wa mazingira katika mikoa mbalimbali aliyofanikiwa kupita hali iliyomsikitisha na kusababisha aiunue kalamu yake na kuandika ujumbe huu wa kutukumbusha kuwa mazingira yetu ni jambo muhimu katika kuleta ustawi wa binadamu.

Uharibifu wa mazingira si tu unaleta ukame na ukosefu wa maji katika miji yetu bali unakwamisha shughuli za uzalishaji katika viwanda na hivyo kudumaza uchumi wetu hali ambayo itashusha kipato katika ngazi ya familia.

Mpita njia anawakumbusha kuwa kumekuwa na vimbunga, mafuriko na majanga yanayoendana na hayo ikiwemo vipindi virefu vya ukame katika mataifa mbalimbali hapa duniani, jukumu letu kwa sasa ni kuepuka athari wanazopata wenzetu kila uchao kwa sababu ya uharibifu wa mazingira  kwa kuacha tabia zinazopelekea hali hiyo.

Ni wakati sasa Mamlaka zote, wananchi na  wadau wa Mazingira tuungane na kukemea vikali uharibu wa mazingira katika maeneo yetu na pia kuchukua hatua ikiwemo ya kupanda miti.

Viongozi mliotakiwa kuhakikisha wafugaji  na wakulima waliopo kwenye vyanzo vya maji wanaondoka ni wakati sasa wa kulisimamia hili kikamilifu ili kulinusuru Taifa na hali hii ya uharibifu wa mazingira



# Rais Samia Awaahidi Maji Wananchi wa Kisongo

**Na Elinipa Lupembe - ARUSHA DC**

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amewaahidi wananchi wa Kisongo, kuwasiliana na wizara ya maji kuona namna ya kuunganisha mradi wa maji wa bilioni 600 wa Jiji la Arusha ili kuwafikia wananchi hao.

Mhe. Rais ameyasema hayo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye soko la Kisongo kata ya Mateves, Halmashauri ya Arusha, Wilaya ya Arumeru, wakati akiwaaga wananchi wa Mkoa wa Arusha mara baada ya kumaliza ziara yake mkoani humo.

"Tumemaliza tatizo la maji Jiji la Arusha kupitia mradi wa maji wa Bilioni 600, mahitaji ya Jiji la Arusha ni lita milioni 90 tu, na maji hayo yamezidi, tutafanya mpango kuhakikisha maji hayo yanaunganishwa hapa, ili wananchi wa Kisongo mpate maji, Kisongo maji yatapatikana". Amesema Mhe. Rais

Mhe. Rais amewahakikishia wana Kisongo maji na kuongeza kuwa wizara ya maji inatekeleza miradi mingi kwa sasa, ikitokea bakaa yoyote ipelekwe Arumeru ili kumaliza tatizo hilo.

Katika mkutano huo, mbunge wa jimbo la Arumeru Magharibi, Mhe. Noah Lembris amemshukuru na kumpongeza Mhe. Rais kwa serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo jimboni humo.

"Kupitia TARURA tumepokea bilioni 1.5 za ujenzi wa barabara za ndani, umesaini mkataba wa bilioni 22 za ujenzi wa barabara ya lami KM 18 Mianzini, Timbolo-Ngaramtoni, milioni 450 kumaliza zahanati 11 lakini pia tumepokea milioni 760 za ujenzi wa madarasa 38 za shule 15 za sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023". Amebainisha Mhe. Noah.

Hata hivyo Katibu Mkuu TAMISEMI Prof. Riziki Shemdoe ameitaja mikakati ya ujenzi wa barabara za ndani katika halmashauri hiyo na kusema kuwa serikali itazingatia mahitaji yaliyowasilishwa na kuweka kwenye mpango wa bajeti kwa mwaka ujao wa fedha.

**Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Nape Nnauye, Leo Novemba 28 2022 amempokea Waziri mwenye dhamana ya masuala ya TEHAMA wa Uganda Mhe. Godfrey Baluku Kabbyanga aliyewasili nchini kwa ziara ya kikazi.**







# Bilioni 1.8 Kuleta Mapinduzi ya Mawasiliano Ludewa

**Na Immaculate Makilika - MAELEZO, Ludewa**

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mhandisi Kundo Mathew amesema kuwa Serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali katika kutatua changamoto za mawasiliano nchini, ambapo katika Wilaya ya Ludewa, mkoani Njombe inatarajia kutumia shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano.

Mhandisi Kundo amesema hayo jana Novemba 27, 2022 katika Kijiji cha Mawengi kilichopo wilayani humo wakati akiwa katika ziara yake ya kukagua miundombinu ya miradi ya mawasiliano, usikivu wa TBC na miradi ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

"Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 1.8 zitakazotumika kwa ajili ya kujenga minara katika kata sita za Iwela, Ludende, Monde, Milo, Mawengi na Lujelawa, huu ni uwekezaji mkubwa utakaofanywa na Serikali ambao utatatua changamoto za mawasiliano katika wilaya hii". Amesema Mhe. Naibu Waziri Kundo.
Ameongeza kuwa tayari kata hizo Sita zimeingizwa katika mfumo wa kutafuta mzabuni kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kutatua changamoto ya mawasiliano katika Jimbo la Ludewa, ambapo katika Kata ya Ibumi ulipo mnara wa TTCL jitihada zinafanyika ili pia mnara huo uweze kutoa huduma.

Akifafanua faida za uwepo wa minara hiyo ya mawasiliano, Mhe. Naibu Waziri huyo amesema "Baada ya miradi hiyo kukamilika mtapata huduma za kupiga simu, kutuma ujumbe mfupi pamoja na intaneti hivyo mtaweza kujifunza masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya biashara na muhimu zaidi ni kuwa, mawasiliano haya ni muhimu hasa katika maeneo haya ya mpakani".

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Mhe. Joseph Kamonga ameishukuru Serikali kwa kuendelea kufanya jitihada mbalimbali za kutatua changamoto ya mawasiliano katika Jimbo la Ludewa.

"Tumeweza kupata mnara kutoka katika Kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya Airtel katika maeneo ya Ilawa na Mkongebaki, vilevile mnara wa Kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya Tigo katika maeneo ya Mkomeng'onde na Ngalawale kwa kipindi hiki kifupi tumepata minara nane, naishukuru sana Serikali hivyo tunaamini baada ya ujenzi wa minara mingine iliyosalia huduma za mawasiliano zitapatikana vizuri zaidi hapa Ludewa na kufungua fursa mbalimbali". Ameeleza Mhe. Kamonga.

Mkazi wa Ludewa, John Edmund ameeleza kuwa wananchi wa eneo hilo wamefurahishwa na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali za kuboresha huduma ya mawasiliano wilayani humo.

"Hakuna aliyetegemea eneo hili la pembezoni kama litakuwa na mawasiliano, hii ni kama ndoto tunaishukuru Serikali kwani tutaweza kuwasiliana vizuri zaidi pamoja na kufahamu taarifa za masuala mbalimbali yanayoendelea ya kitaifa na kimataifa". Ameeleza Bw. Edmund.



# Wilaya 63 Kujengewa VETA

**Na Mwandishi Wetu**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema mageuzi ya elimu yanayokuja yanakwenda sambamba na kuandaa mazingira ya kuhakikisha elimu ujuzi inapatikana.

Mhe. Mkenda ameyasema hayo jijini Dodoma wakati wa kikao cha pamoja cha menejimenti cha wizara na VETA chenye lengo la kujadili kwa pamoja rasimu ya mkakati wa utekelezaji wa ujenzi wa VETA 63 za wilaya na moja ya mkoa.

Amesema moja ya eneo linaloangaliwa katika kutoa elimu ujuzi ni kupitia vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) hivyo ni vizuri kuwa na mikakati thabiti ya kuhakikisha VETA 63 za wilaya na moja ya mkoa ujenzi unaanza.

"Nataka twende pamoja, katika kuweka historia hii, tunakwenda kufanya mageuzi makubwa ya elimu kwa kuhakikisha tunatoa elimu ujuzi, sasa kazi ya mapitio ya sera na mitaala inakwenda vizuri na tuko tayari kufanya wasilisho kwa ajili ya mjadala wa kitaifa, nataka huku kwenye ujenzi wa VETA 63 ambako elimu ujuzi inapatikana kuende kwa kasi na kwa wakati," amesema Prof. Mkenda

Amesema katika mwaka wa fedha 2022/23 wizara imetenga shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa VETA hizo, hivyo kutaka mkakati wa kuhakikisha ujenzi unaanza mapema na kujengwa kwa usahihi kwa kuzingatia taratibu zote husika.

Akizungumzia ujenzi wa kampasi za vyuo vikuu katika mikoa 14 kupitia mradi wa HEET Mhe. Mkenda amewataka Wakandarasi waliopo wizarani kuhakikisha wanafanya ufuatiliaji na kushirikiana na vyuo vikuu kujua mikakati iliyowekwa na vyuo mama kuhusu ujenzi huo ili kazi iweze kwenda kwa haraka.

Naye, Mhandisi George Sambali kutoka VETA amesema mpaka sasa kati ya wilaya 63 zinazojengwa VETA wilaya 59 tayari zina maeneo kwa ajili ujenzi wa VETA.




# Makalla Ahamasisha Wananchi Kuchanja Chanjo ya UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Mhe. Amos Makalla leo amewahamisha wananchi wa mkoa huo kuendelea kujitokeza kuchanja ili kujikinga na UVIKO-19.

RC Makalla ameyasema hayo leo wakati wa matembezi yaliyoandaliwa na hospitali ya Aghakan kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (European Union-EU) kuhamisha wananchi kuchanja dhidi ya Uviko-19.

Aidha RC Makalla amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu chanjo nchini, uamuzi ambao amesema umeokoa vifo, na umesaidia Watanzania kuweza kusafiri nje ya nchi bila tatizo.

Pamoja na hayo RC Makalla amewashukuru hospitali ya Aghakan na EU kwa kufanikisha ukarabati wa wodi ya wazazi hospital ya rufaa ya Amana, mafunzo kwa watendaji wa Afya na elimu ya Uviko-19.

Aidha imeelezwa kuwa, mkoa wa Dar es Salaam umevuka lengo la awamu ya kwanza la kuchanja watu 3,310,000, ambapo mpaka sasa watu waliochanja ni 3,400,000.



# Naibu Waziri Kundo Avuka Ziwa Nyasa Kukagua Vifaa vya Mnara

**Na Immaculate Makilika - MAELEZO**

## Aelekeza Uanze Kutoa Huduma Januari 2023

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mhandisi Kundo Mathew amekagua vifaa vya ujenzi wa mnara wa mawasiliano utakaojengwa na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu za Mkononi ya Tigo katika Kijiji cha Nkwimbili Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe.

Ambapo baadhi ya vifaa alivyokagua ni pamoja na nondo, taa za mnara, miguu ya mnara, jenereta, mtambo wa kudhibiti umeme na betri.

Akihutubia wananchi jana Novemba 27, 2022, katika Kijiji cha Lupingu wilayani humo, Mhe. Naibu Waziri Kundo amesema kuwa lengo la kutembelea mradi huo ni kujua utakamilika lini na huduma watakazopata wananchi.

“Ifikapo Januari 2023, mnara huu utaanza kutoa huduma kwa wananchi na hivyo kutatua changamoto ya mawasiliano katika eneo hili. Wizara tuna miradi ya mipakani na maeneo maalum ili kuhakikisha wananchi wanapata mawasiliano kutoka nchini kwanza, ikiwa ni pamoja na kuchangia uchumi wa nchi kwa manufaa yetu sote," ameeleza Mhe. Naibu Waziri Kundo.

Hata hivyo amewataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano wakati wa ujenzi wa mradi huo pamoja na kuulinda mara utakapoanza kutoa huduma, huku akiwasii kutumia vizuri fursa za mawasiliano watakazopata kutokana na mnara huo.

Kwa upande wake, msimamizi wa mradi wa ujenzi wa mnara katika Kijiji cha Nkwimbili kutoka kampuni ya GNC Solutions LTD, Bw. Suleiman Senga ameahidi kuwa mnara huo utaanza kutoa huduma ifikapo Januari 2023 na kuwa kampuni zingine za simu zinaweza kutumia mnara huyo wa Kampuni ya Tigo kutoa huduma kwa wananchi kupitia kampuni zao.

Kuhusu mnara wa TBC uliopo Milo wilayani humo, Mhe. Naibu Waziri Kundo amesema kuwa kupitia mnara huo vituo vingine vya redio vinaruhusiwa kuweka vifaa vyao ambavyo vitasaidia kuongeza usikivu wa matangazo yao.

Katika hatua nyingine, Mhe. Naibu Waziri Kundo ameielekeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuhakikisha kuwa wanazingatia utaratibu na kuzisaidia kupata leseni kwa haraka redio mbalimbali zilizowasilisha maombi yao ikiwa ni pamoja na redio za halmashauri.



# Tanzania Mwenyeji Warsha ya Kikanda Mpango wa Matumizi ya Eneo la Bahari

**Na Mwandishi Wetu**

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga leo amefungua warsha ya Mafunzo ya Kikanda kuhusu Mpango wa Matumizi ya Eneo la Bahari (Marine Spatial Planning - MSP) na Ukanda wa Pwani ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi katika Hotel ya Protea iliyopo Jijini Dar es salaam.

Amesema lengo la warsha hiyo ni kujenga uwezo wa wataalamu kutoka nchi wanachama wa mkataba wa Nairobi katika kuandaa na kutekeleza mpango wa matumizi ya eneo la bahari, usimamizi wa taarifa za kimazingira, kubadilishana uzoefu na kufahamu hatua zilizofikiwa na nchi wanachama katika kuandaa na kutekeleza mpango wa matumizi ya eneo la Bahari.

Bi. Maganga amesema Tanzania ni mwenyeji wa kikao kazi hicho kinachohusisha wajumbe kutoka zaidi ya nchi 10 wanaotekeleza mkataba wa Nairobi unaohusu hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari na ukanda wa Pwani ya Magharibi.

"Warsha hii imehusisha nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi na nchi zinazoshiriki ni pamoja na Tanzania, Komoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Shelisheli, Re-Union na Afrika Kusini". Alisisitiza Bi. Maganga.

Amesema warsha hiyo itasaidia kuja na mpango na usimamizi endelevu wa matumizi ya rasilimali za bahari ikiwa ni pamoja na mgawanyo sahihi wa matumizi ya bahari.

Aidha ameendelea kusema kuwa, Tanzania inajipanga mapema katika kuandaa mpango huo kwa kuzingatia kuwa uchumi wa bluu ni miongoni mwa agenda za Dunia.

"Ninapozungumzia uchumi wa bluu ninasisitiza usimamizi endelevu na shirikishi wa mifumo ikolojia ya Pwani na bahari ya Tanzania ili kuendelea kutoa bidhaa na huduma muhimu ikiwa ni pamoja masuala ya uvuvi na uchimbaji wa mafuta na gesi pale vitakakapogundulika". Alisisitiza Bi. Maganga

Warsha ya mafunzo ya kikanda kuhusu Mpango wa Matumizi ya Eneo la Bahari (Marine Spatial Planning - MSP) na Ukanda wa Pwani Magharibi mwa Bahari ya Hindi na Kujenga Uwezo Katika Usimamizi wa Taarifa za Mazingira imeanza leo tarehe 28 Novemba na inatarajia kukamilika 1 Disemba 2022. Warsha hii inafanyika katika Hotel ya Protea Jijini, Dar es Salaam.

Maelezo



# Mradi wa Majisafi Tanga Wafikia Asilimia 72

**Na Jmala Zuberi - Tanga**

Mradi wa kuboresha huduma ya majisafi Tanga awamu ya Pili ikiwa ni pamoja na kazi za ujenzi na usambazaji wa vifaa umefikia asilimia zaidi 72.

Mradi huo unalenga kukidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji la Tanga na miji ya Muheza na baadae kuwa chanzo cha maji kwa maeneo ya Kasera na Horohoro wilayani Mkinga.

Hayo yamesemwa na Mhandisi wa mradi huo Elikana Kayungilo wakati akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga Omary Mgumba alipotembelea kukagua mradi huo.

"Mradi huu utaongeza uwezo wa usafirishaji na usambazaji maji kwa kulaza bomba kubwa lenye kipenyo cha milimita 600 kutoka kituo cha kusafisha na kutibu maji Mowe hadi kwenye tangi kuu la Kange jijini Tanga," alifafanua Elikana.

Amesema baada ya utekelezaji wa mradi huo kiasi cha maji yanayowafikia wananchi wa Jiji la Tanga na mji wa Muheza kwa mita za ujao 15,000 kwa siku na kufanya uwezo wa uzalishaji maji kupanda kutoka mita 30,000 hadi 45,000 za ujazo.

Mradi huu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga (TangaUwasa) unatarajiwa kugharimu kiasi cha Bilioni 9.180, umeanza utekelezaji Septemba 2021 na unatarajia kukamilika Desemba 2022.



# Mkurugenzi Mkuu PSSSF Apata Tuzo ya Mtendaji Mkuu Bora wa Taasisi za Umma 2022

**Na Mwandishi Wetu - Dar es Salaam**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), CPA. Hosea Kashimba, amepata tuzo ya kuwa Mtendaji Mkuu Bora wa mwaka 2022 kwa upande wa Taasisi za Umma nchini.

Utoaji wa tuzo hizo uliratibiwa na taasisi ya kimataifa ya KPMG yenye uzoefi wa miaka 35 katika masuala ya Bima, Fedha, Sheria na Kodi. Tuzo hizo zilitolewa hivi karibuni katika ukumbi wa mikutano wa Mlimani City, Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na watu mbalimbali wakiwemo watendaji wa taasisi mbalimbali.

Akizumgumza baada ya kupokea tuzo hiyo, CPA. Kashimba alisema, "naelekeza tuzo hii kwa wanachama wa PSSSF, hii ni zawadi yao ya kufungia mwaka, hakika tuzo hii inanipa nguvu ya kuwatumikia vyema zaidi wanachama kwa mwaka 2023".

CPA. Kashimba ni mhitimu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe ambako alitunukiwa Shahada ya Uzamili katika Uongozi wa Biashara (MBA Corporate), pia amesomea uhasibu katika Chuo cha Maendeleo ya Uongozi (IDM Mzumbe) na kuhitimu Stashahada ya juu ya Uhasibu. Vilevile amehudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

CPA. Kashimba ni mwanachama wa Institute of Directors Tanzania (IoDT) na mjumbe wa Bodi kwenye taasisi mbalimbali ikiwa pamoja na Benki ya CRBD. Kabla ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, ameshakuwa Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani katika uliokuwa Mfuko wa Pensheni wa PPF.

CPA. Kashimba aliteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF kuazia tarehe 19 Februari, 2019.
KPMG hutumia vigezo vingi ikiwemo uongozi bora na unaoacha alama katika sehemu unayoongoza na kwa jamii kwa jumla ili kuweza kumpata mtendaji bora.

Maelezo

2022.MAELEZO PODCASTS.



# SIKILIZA PODCASTS ZA KISWAHILI KUTOKA IDARA YA HABARI MAELEZO.

2022.MAELEZO PODCASTS.

## MAELEZO PODCASTS

Tunapatikana: Spotify, Apple Podcasts, Google Podcasts, Amazon music, Stitcher iHeartRadio, Pandora, TuneIn + Alexa, Podcast Addict, Podchaser, Pocket Casts, Overcast, Castro, Castbox, Podfriend, Deezer, Listen Notes, Player FM, Podcast Index Podcast Index, AudioMack, Soundcloud

MSEMAJIMKUUWASERIKALI/MAELEZONEWS/
WWW.MAELEZO.GO.TZ